

# Kuhusu nguo kwenye chekechea



## NGUO

Katika chekechea, mtoto anapaswa kuva nguo ambazo hamuogopi kama zinaweza kuchafuliwa au kuharibiwa. Nguo zinapaswa kuwa rahisi kuva na kuvua, na starehe kwa mtoto akicheza na kutembea. Huku Bergen, kuna mvua nyingi na hali ya hewa hubadilika mara kwa mara, na inaweza kuwa vigumu kuwalisha watoto sawa. Watoto hawapaswi kuganda juu ya baridi, lakini wanashughulika nje na hawapaswi kuva nguo nyingi sana ambazo zinazua kucheza na kutumbea huru. Wafanyakazi katika chekechea wanaweza kukusaidia kuchagua nguo ambazo zinaffaa kulingana na hali za hewa tofauti.

### Uwekaji wa alama kwenye nguo

Ili kuhakikisha kuwa mtoto ameleta nguo sawa nyumbani, unapaswa kuweka alama ya majina kwa nguo zote. Vitambulisho vya majina ambavyo vinabandikwa upande wa ndani ya nguo vinaweza kuagizwa kwa mtando. Nguo zinaweza pia kuwekwa alama kwa kutumia kalamu ya wino kuzuia maji isifute.

### Je! Mtoto anahitaji nguo gani huko chekechea?

Mtoto anahitaji nguo za mvua na buti wakati kunanyesha au kuna mvua nyingi nje. Ni muhimu kuwa na seti ya nguo za mvua zilizoanikwa kwenye chekechea. Ikiwa nguo za mvua zimechafuka, zinapelekwa nyumbani na kuoshwa.

Ni lazima mtoto avae viatu vya ndani au sandale kila siku. Sakafu inaweza kuwa yenye utelezi na mtoto anaweza kuteleza ikiwa anatembea kwa soksi. Inaweza pia kuwa maji kwenye sakafu, na mtoto anaweza kupata maji kwa miguu ikiwa havai viatu vya ndani au sandale.





© Trude Haugen



© Trude Haugen



© Nina Horningsvåg Traet

## Nguo za ziadi

Ni kawaida kuwa watoto hulowa maji au kupata uchafu wanapocheza katika chekechea. Kwa hivyo watoto wanahitaji kubadilisha nguo. Ni muhimu kuwa na nguo za ziada zilizowekwa huko chekechea, kama vile chupi, soksi, suruali ndefu ya ndani, sweta na suruali. Angalia mara kwa mara ikiwa mtoto ana kile kitu kinachohitajika kwa nguo za ziada.

## Katika msimu wa joto

Wakati hali ya hewa inakuwa joto, mtoto anahitaji nguo nyepesi na viatu vyepesi. Katika msimu wa chemchemi au vula inafaa kuva kofia nyembamba na ikiwezekana mavazi ya bustani bila sufu. Wakati kuna jua kali nje, mtoto anapaswa kuleta mafuta ya kujikinga kwa jua kali. Zaidi, inashauriwa kuva kofia ya jua au kofia ya kulinda kichwa.



© Trude Haugen

Picta © Nina Hornningsvåg Traet

© Marie Rosenvinge

Svanemerket tryksak, 2041 0713

Skipnes.no

## Katika msimu wa baridi

Wakati kuna baridi nje, mtoto anahitaji suti ya baridi. Ndani ya suti hiyo anaweza kuva sweta na suruali ya sufu au ngozi. Vinginevyo, ni muhimu kuwa na kofia ya joto, soksi za sufu, viatu vya joto na visivyoingiza maji, na kinga za baridi za mikono.

Kumbuka kwamba mara nydingi kinga za mikono hulowa maji, kwa hivyo unaweza kuleta kadhaa.

## Mavazi wakati mtoto analala nje kwenye gari ya kumsukuma

Watoto wadogo wanahitaji kupumzika wakati wa mchana. Katika chekechea zingine, watoto wanalala nje kwa gari ya mtoto kwa usimamizi wa wafanyakazi. Ni muhimu kuwa na begi la gari, ili mtoto asivae nguo nydingi. Ndani ya begi la gari, ni vizuri kuweka nguo nyembamba za sufi hata ikiwa ni wakati wa baridi.

Ongea na wafanyakazi katika chekechea ikiwa una maswali yoyote kuhusu kulala kwenye gari la kusukuma mtoto

## Mengine

Watoto ambao wanaotumia nepi, pampas, mpira wa kunyonya, mafuta yoyote ya utunzaji lazima hii iwekwe katika chekechea.



BERGEN  
KOMMUNE